



GIRLS' VISION

kuhusu Elimu

MACHI
2025

Muhtasari wa Hoja Kuu

Kutekeleza hatua za kutimiza mahitaji
na vipaumbele vya elimu kwa wasichana

MALALA FUND

Muhtasari wa Hoja Kuu

Dira yetu kuhusu elimu huwaruhusu wasichana kupata maisha bora, heshima na kuwa tayari kwa ajili ya mambo mengi zaidi na kugundua nafasi yao duniani.

— Maelezo ya dira kutoka kwenye warsha iliyofanywa pamoja na wasichana wenye umri wa chini ya miaka 13 wanaoenda shule nchini Brazili



Huku mapitio muhimu yakiendelea kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) na Azimio la Beijing na Jukwaa la Utekelezaji, ajenda mbili kuu za kimataifa za kuendeleza elimu bora na haki za wanawake na wasichana, 2025 ni mwaka muhimu wa kupima maendeleo yaliyofanywa kuelekea kupata **usawa wa kijinsia** katika elimu. Malengo ya Maendeleo Endelevu yanategemea viwango vya **ulinganifu wa kijinsia** — hasa uwiano wa wavulana na wasichana wanaoandikishwa shuleni na wanaomaliza shule — ili kupima maendeleo katika eneo hili. Ingawa data inaonyesha kuwa ulimwengu ulitimiza lengo hili mnamo mwaka 2013, ukosefu wa usawa wa kijinsia katika elimu bado umeenea katika nchi zenye kipato cha chini.¹ Wasichana vijana hasa wanakabiliwa na aina nyingi zinazolingiliana za ubaguzi unaohusiana na umri na jinsia — unaochangiwa na umaskini — unaowazuia kupata elimu na kumaliza miaka 12 ya elimu hiyo.²

Leo, wasichana vijana milioni 88 wameacha shule ya sekondari, na mamilioni wengine hawapati elimu salama na bora inayowapa maarifa na ujuzi wanaohitaji ili wafanikiwe.^{3,4} Wasichana wanajua wanachotaka hasa katika elimu yao — serikali na taasisi za kimataifa lazima ziwasikilize, kuchukua hatua ili kuendeleza usawa wa kijinsia shuleni na kutimiza haki ya kupata elimu ya sekondari kwa wasichana wote.



Malala Fund inatambua kwamba ili kuelewa kile ambacho wasichana wanahitaji katika elimu yao, tunahitaji kuwauliza.

Katika Kongamano la Usawa wa Vizazi la mwaka 2021, tulijizatiti kuunda dira mpya ya elimu tukishirikiana na wasichana — ambayo ingetimiza mahitaji na mambo wanayotamani kupata.⁵ Ili kuendeleza ahadi hii, tuliandaa mashauriano ya **Dira ya Wasichana kuhusu Elimu** ili kupata maoni hasa kutoka kwa wasichana wasiopata rasilimali za kutosha, tukishirikiana na wasichana hao moja kwa moja katika mchakato mzima. Zaidi ya wasichana 800 kutoka nchi 30 walitoa maoni muhimu kuhusu changamoto zao na vipaumbele vyao vya elimu ya sekondari. Tulisikia kuwa:

1. **Wasichana wanataka elimu inayowapa uwezo wa kujitegemea na kuwawezesha.** Wanaazimia kupata maarifa, ujuzi na fursa kupitia elimu ili kuwasaidia kujitegemea na kujiamini na kuleta mabadiliko katika jamii.
2. **Wasichana wanataka kujifunza katika shule zinazofaa kwa karne ya 21 ambapo wanapata heshima.** Wanatamani elimu isiyo na ubaguzi, inayowaruhusu kujieleza kwa ubunifu na kutoa fursa za kujifunza mada zinazowavutia na kuwaandaa kushiriki kikamilifu katika maisha ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.
3. **Wasichana wanataka serikali zitimize ahadi za kupunguza vikwazo katika elimu yao.** Serikali zinapaswa kuweka kipaumbele kwenye hatua za kukabiliana na vikwazo vya kifedha, ikatili wa kijinsia na utoaji duni wa huduma za kutimiza afya na usafi wakati wa hedhi ambao huwazuia wasichana kwenda shuleni na kumaliza shule.

Dira yetu ya elimu itaruhusu [wasichana] kujiamini na kuzungumza kwa ujasiri. Kila msichana hupata fursa ya kumaliza elimu yake vizuri ili kusiwe na wanafunzi walioacha shule kama sisi. Tunataka mfumo wa elimu ambapo wasichana wanaweza kujifunza kwa uhuru na bila matatizo.

— Maelezo ya dira kutoka kwenye warsha iliyofanywa pamoja na wasichana walio na umri wa chini ya miaka 13 ambao hawaendi shule nchini Bangladesh



Serikali na taasisi za kimataifa hazipaswi kupuuza madai ya wasichana ya kufanya mabadiliko na zinahitaji kushirikiana na wasichana ili kufikia maono yao ya elimu na kutekeleza haki za wasichana. Malala Fund ilishirikiana na wasichana, viongozi vijana wa wanawake na mashirika washirika wa Girls' Vision ili kubaini maeneo matano makuu yanayohitaji hatua kuchukuliwa:

- 1. Kutimiza ahadi zilizopo za kimataifa kwa wasichana kwa kuongeza uwekezaji na kuimarisha viwango vya elimu vya kitaifa.** Wasichana wanataka serikali ziongeze pesa zinazotumika kwenye elimu katika vipaumbele vyao na kuimarisha mifumo ya kitaifa ya sheria na sera ili kuhakikisha elimu salama na bora inayokidhi vyema zaidi mahitaji na mambo ambayo wasichana wote wanatamani kupata.
- 2. Kuwapa rasilimali wasichana wanaoongoza mabadiliko katika jamii zao.** Wasichana huleta mabadiliko katika jamii zao na wanahitaji ufadhili na rasilimali bora za kufadhili harakati na mipango yao ya kuboresha elimu kwa wasichana wote.
- 3. Kuwatengea wasichana nafasi katika michakato ya kitaifa na kimataifa ya kufanya maamuzi na kuunda sera kuhusu elimu.** Ushiriki muhimu wa wasichana katika michakato ya kufanya maamuzi ni muhimu katika kuhakikisha kuwa mifumo na michakato ya elimu inawafaa zaidi.
- 4. Kuweka kipaumbele katika viashiria vya elimu kuhusu usawa wa kijinsia.** Kwa kuzingatia ulinganifu wa kijinsia bila uwiano, watunga sera wa kimataifa hawapimi kwa ufanisi maendeleo ya elimu ya wasichana. Ni lazima waweke kipaumbele zaidi kwenye viashiria vya usawa wa kijinsia. Tazama kadi za ripoti za elimu ya wasichana za Malala Fund.⁶
- 5. Kupiga jeki juhudi za kushughulikia ukatili wa kijinsia unaohusiana na shule, kukuza afya wakati wa hedhi na kuimarisha ufikiaji na elimu ya kidijitali kwa wasichana.** Serikali na taasisi za kimataifa lazima ziongeze uwekezaji katika maeneo haya, ambayo yaliibuka kama vipaumbele maalum vya wasichana katika mchakato wa mashauriano.





Malala Fund inawashukuru mno mamia ya wasichana walioshiriki katika mchakato wa mashauriano na wale walioshirikiana nasi moja kwa moja kuwasilisha taarifa zilizo katika ripoti hii. Tulisoma kila jibu, bango la warsha na maoni.




Muhtasari wa mashauriano

Wasichana hao ni akina nani?

Wasichana 810 kutoka nchi 30:

- Warsha: Wasichana 482 kutoka nchi 12 katika warsha 76
- Utafiti: Wasichana 328 kutoka nchi 25



Kiwango cha elimu rasmi

Hali ya ulemavu

Wasichana 159:
asilimia 20 ya
wote waliojibu



Wasichana wanataka —

Elimu inayowapa uwezo wa kujitegemea na kuwawezesha

- **Asilimia 38** ya Maelezo ya Dira ya Wasichana ilitaja wasichana kuthaminiwa katika jamii na kuwasaidia wengine
- **Asilimia 64** ya wasichana katika utafiti walisema dira yao kuhusu elimu itawawezesha wasichana kudhibiti maisha yao ya baadaye

Shule za karne ya 21 ambapo wanaheshimiwa

- Wasichana walitanguliza masomo ya ubunifu, ujuzi wa kukabiliana na changamoto za maisha na elimu ya kidijitali
- **Asilimia 40** ya Maelezo ya Dira ya Wasichana kuhusu elimu ilitaja ujumuishaji, usalama na heshima
- **Asilimia 15** ya wasichana katika utafiti walitoa wito hasa wa kutolewa kwa elimu inayojumuisha watu wote na inayozingatia jinsia

Serikali kutekeleza ahadi za kupunguza vikwazo, hasa

- **Vikwazo vya kifedha** — vilitajwa katika asilimia 67 ya warsha
- **Kukomesha dhuluma za kijinsia zinazohusiana na shule** — kipaumbele cha 2 kwa wasichana wote

Kwamba msichana ana uwezo wa kujitegemea kifedha kiasi kwamba anaweza kuwasaidia watu wa familia yake na kuwasaidia wazazi wake kwa kutoa mchango wa kifedha nyumbani. Aidha, kwa kufanya hivi, katika siku zijazo anaweza kuhudumu kama njia ya kukuza kizazi kinachojitegemea zaidi kifedha.

- Maelezo ya dira kutokakwenye warsha iliyofanywa na watu wenye umri wa miaka 14-16 ambao wanaenda shule nchini Pakistan




Maswala ya Kuangaziwa

- **Asilimia 59** ya wasichana walisema kwamba wasichana wenyewe wana uwezo mkubwa zaidi wa kuboresha elimu – zaidi ya serikali (asilimia 39)
- **Asilimia 40** ya wasichana walitoa wito wa kudumisha afya na usafi wakati wa hedhi ili kuboresha elimu – kipaumbele cha kwanza
- Elimu ya kidijitali na uelewa ulikuwa kipaumbele dhahiri kwa wasichana katika majibu ya warsha na utafiti

Marekebisho ya elimu!

Jinsi ambavyo wasichana wangetenga fedha za bajeti za elimu

- Utoaji wa huduma: majengo ya shule, maeneo ya huduma (USAFI haujajumuishwa)
- Msaada wa kifedha kwa wasichana/familia
- Usalama
- Ya pamoja/mahususi Inayozingatia Jinsia (zote)
- Mabadiliko mapana ya kijamii/ kushirikisha jamii
- Mengineyo



- | | |
|------------------|------------------|
| • Asilimia 54.17 | • Asilimia 14.97 |
| • Asilimia 21.07 | • Asilimia 5.03 |
| • Asilimia 4.23 | • Asilimia 0.53 |





Muhtasari wa mashauriano: Wasichana wasiohudhuria shule

Wasichana hao ni akina nani?

Wasichana 229:

- Wasichana 144 kutoka nchi 8 (warsha 22)
- 85 kutoka nchi 7



Hali ya ulemavu

Wasichana 35: asilimia 42 ya wasichana wa OOS (utafiti)

Utafiti (idadi=wasichana 86)



Wasichana wanataka —

Elimu inayowapa uwezo wa kujitegemea na kuwawezesha

- **Asilimia 41** ya Maelezo ya Dira ya Wasichana wa OOS ilitaja kujifunza ujuzi muhimu (asilimia 41). Kukuza kujiamini (asilimia 36) na kukuza thamani ya wasichana na kuheshimiwa katika jamii (asilimia 36) pia kulitajwa mara nyingi.
- **Asilimia 71** ya wasichana wa OOS katika utafiti walisema maono yao ya elimu yatawawezesha wasichana kudhibiti maisha yao ya baadaye

Shule za karne ya 21 ambapo wanaheshimiwa

- Katika warsha na wasichana wa OOS, walitanguliza elimu ya kidijitali (asilimia 46) na sanaa za kuigiza/muziki (asilimia 41).
- Katika utafiti huo, walitanguliza ujuzi wa kusoma na kuandika (asilimia 55) na ujuzi wa ubunifu (asilimia 51) kama mada
- **1/4** ya Taarifa za Maono za wasichana wa OOS kuhusu elimu zilitaja ujumuishaji, usalama na heshima

Serikali kutekeleza ahadi za kupunguza vikwazo, hasa

- **Vikwazo vya kifedha** – vilitajwa katika karibu warsha zote (asilimia 91)
- **Kukomesha dhuluma za kijinsia zinazohusiana na shule** — wasichana wa OOS walieleza wasiwasi wao hasa kuhusu uonevu, unyanyasaji wa kingono na njia zisizo salama. Uboreshaji wa njia salama ulikuwa kipaumbele cha uwekezaji na uboreshaji.

Ndoto yangu kuhusu elimu itawapa wasichana fursa ya kutumia haki zao, kuwa wazazi bora kwa watoto wao na kitu cha kujivunia katika jamii.

– Maelzo ya dira kutoka kwenye warsha iliyofanywa pamoja na watu wenye umri wa miaka 14-16 ambao hawahudhuri shule nchini Naijeria




Maswala ya Kuangaziwa

- **Asilimia 58** ya wasichana wa OOS walijiona kuwa wana uwezo mkubwa zaidi wa kuboresha elimu ya wasichana, kuliko familia za wasichana (asilimia 63)
- **Asilimia 31** ya wasichana wa OOS walitoa wito wa kudumisha afya na usafi wakati wa hedhi ili kuboresha elimu – kipaumbele cha kwanza
- Elimu ya kidijitali na uelewa haukuwa kipaumbele kikuu kwa wasichana wa OOS, lakini bado ulikuwa miongoni mwa maswala matatu makuu kuhusu mada, uwekezaji na maboresho

Marekebisho ya elimu!

Jinsi ambavyo wasichana wangetenga fedha za bajeti za elimu

- Utoaji wa huduma: majengo ya shule, maeneo ya huduma (USAFI haujajumuishwa)
- Msaada wa kifedha kwa wasichana/familia
- Usalama
- Ya pamoja/mahususi Inayozingatia Jinsia (zote)
- Mabadiliko mapana ya kijamii/ kushirikisha jamii
- Mengineyo




- | | |
|------------------|-----------------|
| ● Asilimia 54.90 | ● Asilimia 9.13 |
| ● Asilimia 21.75 | ● Asilimia 5.02 |
| ● Asilimia 8.37 | ● Asilimia 0.81 |




Muhtasari wa mashauriano: Wasichana wadogo na wakubwa

Wasichana hao ni akina nani?


- Miaka 8-14 Asilimia 14 (idadi=wasichana 114)
- Miaka 14 - 19 Asilimia 62 (idadi=wasichana 501)
- Miaka 9-25 Asilimia 22.8 (idadi=wasichana 185)




warsha (idadi=warsha 72):



Utafiti (idadi=wasichana 328)



Warsha (idadi=warsha 21)



Utafiti (idadi=wasichana 86)



Wasichana wanataka —

Elimu inayowapa uwezo wa kujitegemea na kuwawezesha

- Katika Maelezo ya Dira (warsha), wasichana wakubwa walionekana kutanguliza uwezo wa kujitegemea na kujikimu kifedha zaidi kuliko vikundi vingine vya umri. Wasichana (14-19) walionekana kulenga kujiamini na kuthaminiwa katika jamii.
- Katika utafiti huo, wasichana wakubwa (miaka 19-24) walitanguliza kutiwa msukumo ili wafikie ndoto zao na wasichana (miaka 16-18) walitanguliza kuheshimiwa zaidi.

Shule za karne ya 21 ambapo wanaheshimiwa

- Katika warsha, wasichana wakubwa (miaka 20-25) walitanguliza kujifunza kuhusu afya ya ngono na uzazi na haki (SRHR) zaidi kuliko vikundi vingine na hawakutaja sanaa za kuigiza hata kidogo (kipaumbele kwa umri mwingine). Wasichana wadogo (miaka 8-13) walitanguliza kujifunza sanaa za ubunifu (50%).
- Katika utafiti, wasichana wakubwa (miaka 19-24) walikuwa na uwezekano mkubwa wa kutaja ujuzi wa kukabiliana na changamoto za maisha na wadogo (miaka 16-18) walikuwa na uwezekano mkubwa wa kutaja ujuzi wa ubunifu.

Serikali kutekeleza ahadi za kupunguza vikwazo, hasa

- **Vikwazo vya kifedha** — kikwazo kikuu kilichotajwa katika warsha zote katika vikundi vyote vya umri
- **Kukomesha dhuluma za kijinsia zinazohusiana na shule** — kulitajwa zaidi na wasichana wenye umri wa zaidi ya miaka 14. Uboreshaji wa njia salama ulikuwa kipaumbele cha uwekezaji na uboreshaji.

Dira yetu kuhusu elimu [yatawaruhusu] wasichana kutotegemea wazazi wao au wanajamii wengine na kuelewa haki za wasichana na nafasi yao katika jamii.

– Maelezo ya Dira kutoka kwenye warsha iliyofanywa pamoja na watu wenye umri wa chini ya miaka 13 wasiohudhuria shule nchini Tanzania




Maswala ya Kuangaziwa


- 62% ya wasichana wadogo na 55% ya wasichana wakubwa walisema wasichana wenyewe wana uwezo mkubwa zaidi wa kuboresha elimu
- 41% ya wasichana wadogo na 39% ya wasichana wakubwa walitoa wito wa kudumisha afya na usafi wakati wa hedhi ili kuboresha elimu – kipaumbele cha kwanza
- Elimu ya kidijitali na uelewa ulikuwa kipaumbele dhahiri kwa wasichana katika vikundi vyote vya umri

Marekebisho ya elimu!


Jinsi ambavyo wasichana wangetenga fedha za bajeti za elimu



Miaka 8–14 (idadi=18)



Miaka 14–19 (idadi=47)



Miaka 19–25 (idadi=7)

- Utoaji wa huduma: majengo ya shule, maeneo ya huduma (USAFI haujajumuishwa)
- Msaada wa kifedha kwa wasichana/familia
- Usalama
- Ya pamoja/mahususi inayozingatia Jinsia (zote)
- Mabadiliko mapana ya kijamii/kushirikisha jamii
- Mengineyo




Muhtasari wa mashauriano: Wasichana wanaoishi na ulemavu


Wasichana hao ni akina nani?

Wasichana 159

- 73 kutoka nchi 2 (warsha 21)
- Wasichana 86 kutoka nchi 17




Warsha (idadi=warsha 21)



Utafiti (idadi=wasichana 86):

Kiwango cha elimu rasmi



Utafiti (idadi=wasichana 86)



Wasichana wanataka —

Elimu inayowapa uwezo wa kujitegemea na kuwawezesha

- Katika Taarifa za Maono (warsha), wasichana wanaoishi na ulemavu (LWD) pia walitanguliza: elimu inayojumuisha watu wote na inayozingatia jinsia; wasichana kuthaminiwa katika jamii na kuwasaidia wengine; kujitegemea na uhuru.
- **Asilimia 74** ya wasichana katika utafiti huo walisema dira yao kuhusu elimu itawasaidia wasichana kudhibiti maisha yao.

Shule za karne ya 21 ambapo wanaheshimiwa

- Katika warsha zilizofanywa pamoja na wasichana wanaoishi na ulemavu, walitanguliza kujifunza sanaa za ubunifu (asilimia 57) na sanaa za kuigiza (asilimia 43) kuliko somo lingine lolote.
- Katika utafiti huo, walitanguliza kujifunza ujuzi wa kushughulikia fedha na biashara kuliko kikundi kingine chochote. Pia walitanguliza uelewa na elimu ya kidijitali.

Serikali kutekeleza ahadi za kupunguza vikwazo, hasa

- Vikwazo vya kifedha (asilimia 43) na majengo yasiyo na huduma na vifaa vinavyowafaa (asilimia 36%) vilitajwa mara kwa mara
- **Kukomesha dhuluma za kijinsia (GBV) zinazohusiana na shule** ndicho kikwazo kilichotajwa mara nyingi zaidi katika warsha, huku wasichana wakitaja uonevu (asilimia 50) na ukatili/unyanyasaji wa kijinsia (asilimia 36) mara kwa mara.

Maono yetu ya Elimu yatawaruhusu wasichana kuwa raia waliowezeshwa na wastahimilivu ambao wanaweza kuongoza [na] kuwashauri wengine kufanya maamuzi yanayokuza maendeleo na kujitegemea.

- Taarifa ya Maono kutoka kwa warsha iliyofanywa pamoja na wasichana wanaoishi na ulemavu walio na umri wa miaka 14-16 na wanaohudhuria shule nchini Kenya




Maswala ya Kuangaziwa

- **Asilimia 55** ya wasichana wanaoishi na ulemavu walijiona kuwa wana uwezo mkubwa zaidi wa kuboresha elimu ya wasichana huku familia za wasichana zikiwa za pili (asilimia 45)
- **Asilimia 44** ya wasichana wanaoishi na ulemavu walitoa wito wa kudumisha afya na usafi wakati wa hedhi ili kuboresha elimu - kipaumbele cha kwanza
- Elimu ya kidijitali na uelewa ulikuwa kipaumbele dhahiri kwa wasichana wanaoishi na ulemavu katika majibu ya warsha na utafiti

Marekebisho ya elimu!

Jinsi ambavyo wasichana wangetenga fedha za bajeti za elimu

- Utoaji wa huduma: majengo ya shule, maeneo ya huduma (USAFI haujajumuishwa)
- Msaada wa kifedha kwa wasichana/familia
- Usalama
- Ya pamoja/mahususi Inayozingatia Jinsia (zote)
- Mabadiliko mapana ya kijamii/ kushirikisha jamii



- Asilimia 29.41
- Asilimia 35.21
- Asilimia 22.35
- Asilimia 5.67
- Asilimia 7.34

Mependekezo

Kupitia Girls' Vision for Education, Malala Fund ilifanya juhudi za kupata maoni na vipaumbele kutoka kwa wasichana na kushirikiana nao kuunda mpendekezo yetu. Viongozi vijana wa wanawake na washirika wa Girls' Vision waliwezesha mchakato wa uthibitishaji wa Malala Fund. Kupitia mchakato huu, kwa pamoja tulitambua mpendekezo muhimu ya sera kwa serikali na taasisi za kimataifa ili kusaidia kutimiza maono ya wasichana kuhusu elimu.

- **Kutimiza ahadi za kimataifa kwa wasichana kwa kuongeza uwekezaji na kuimarisha viwango vya elimu vya kitaifa.** Wasichana wanafahamu mapengo yaliyopo kati ya viwango vya kimataifa na utekelezaji wa serikali zao. Wanataka serikali kuongeza bajeti za elimu na kuimarisha mifumo ya kitaifa ya sheria na sera ili kutoa miaka 12 ya elimu ya bure, salama na bora inayokidhi vyema zaidi mahitaji na mambo ambayo wasichana wote wanatamani kupata. Wanaomba hatua zichukuliwe na serikali ili kusaidia vikundi visivyolindwa vya kutosha na viwango vya kimataifa na kitaifa, kama vile wasichana wajawazito au ambao ni wazazi, wasichana wanaoishi na ulemavu na wasichana wanaolazimishwa kuolewa wakiwa watoto.
- **Kutoa rasilimali za kuwezesha uanaharakati wa wasichana.** Wasichana huleta mabadiliko katika jamii zao lakini wanahitaji upatikanaji zaidi wa ufadhili na rasilimali bora za kufadhili harakati na mipango yao ya kuboresha elimu.⁷ Licha ya ongezeko la wito wa kuongeza ufadhili kwa mashirika ya wasichana na yanayoongozwa na vijana, na huku vijana wakiwakilisha asilimia 25-30 ya watu katika nchi zenye mapato ya chini na kati, ni asilimia 5.6 tu ya ufadhili rasmi wa maendeleo ulimwenguni (ODA) uliolenga maswala ya jinsia na vijana katika mwaka wa 2020.⁸
- **Kuwatengea wasichana nafasi katika michakato ya kitaifa na kimataifa ya kufanya maamuzi na kuunda sera kuhusu elimu.** Ushiriki muhimu wa wasichana katika michakato ya kufanya maamuzi ni muhimu ili kuhakikisha kuwa sera na utendaji wa kielimu, na utekelezaji wake, unawafaa. Mifano ya utendaji mzuri ni pamoja na kufanya mashauriano muhimu na vikundi na mitandao inayoongozwa na wasichana au vikundi vya pamoja na vilivyopangwa vya wanafunzi; kukiwa na asilimia ya nafasi zilizotengewa wasichana miongoni mwa wajumbe wa kitaifa katika michakato ya sera ya elimu ya kimataifa; na mashirika muhimu ya ushauri wa wasichana ya kitaifa yenye rasilimali za kutosha.
- **Kuweka kipaumbele katika viashiria vya elimu kuhusu usawa wa kijinsia.** Kwa kuzingatia ulinganifu wa kijinsia bila uwiano, watunga sera wa kimataifa hawapimi kwa ufanisi maendeleo ya elimu ya wasichana. Ni lazima waweke kipaumbele zaidi kwenye viashiria vya usawa wa kijinsia, hasa hatua za kisera za kuondoa vikwazo vya kifedha kwa elimu, kushughulikia ukatili wa kijinsia unaohusiana na shule na kulinda na kukuza haki za wasichana. Tazama kadi za ripoti za elimu ya wasichana za Malala Fund.^{9 10}
- **Kupiga jeki juhudi za kushughulikia ukatili wa kijinsia unaohusiana na shule, kukuza afya na usafi wakati wa hedhi na kuimarisha elimu ya kidijitali.** Wasichana walitoa hasa kipaumbele kwa maeneo haya kupitia mchakato wa mashauriano. Serikali na taasisi za kimataifa lazima ziongeze uwekezaji katika maeneo haya, kwa kuangazia hasa usalama wakati wa kuelekea na kuondoka shuleni na ndani ya shule, kukuza afya na usafi wakati wa hedhi na kuimarisha elimu ya kidijitali na uelewa kwa wasichana.

Utambuzi

Malala Fund inawashukuru sana wasichana wote 866 ambao walitupatia muda na maoni yao katika mchakato wa mashauriano. Pia tunawashukuru wasichana 45, viongozi vijana wa wanawake na wawezeshaji wa warsha ambao waliendesha mchakato wa uthibitishaji.

Kwa uongozi na ushirikiano wao, tunatoa shukrani kwa:

Viongozi wa Girls' Vision: Meti Gemechu, Ayesha Kareem na Tamilore Omojola

Kamati ya uongozi ya Girls' Vision: Antara, Elizabeth, Hasna, Lauryn na Miriam

Washirika wa Girls' Vision: AfyaPlus, Girl Child Africa Foundation & Save the Children South Sudan, Roots and Wings ELIXIR, World Association of Girl Guides and Girl Scouts (WAGGGS), World YWCA na Zindagi Trust.

Mshirika wa kiufundi: Here I Am

Pia tunatambua uongozi na juhudi za Ines Goncalves, Jean-Ann Ndow na Mashal Hussain.

Tunashukuru kwa kujitolea kwa Echidna Giving kwa elimu ya wasichana na kuwezesha kazi hii muhimu.

Mwandishi: Carron Mann

Wahakiki: Lucia Fry na Gayatri Patel

Mhariri: Emilie Yam

Usanifu: Jianan Liu

Utambuzi wa umiliki wa picha:

Ukurasa wa 2, World Association of Girl Guides and Girl Scouts (WAGGGS)
Ukurasa wa 5, AfyaPlus Organization
Ukurasa wa 15, World Association of Girl Guides and Girl Scouts (WAGGGS)

Endnotes

1. UNESCO (2024) *#HerEducationOurFuture: Investing in girls' and women's education: a smart investment to accelerate development; the latest facts on gender equality in education* <https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pt0000388934>
2. Malala Fund (2023) *Making the grade: Girls' education report cards*. <https://reportcards.malala.org/>
3. UNESCO (2023) *Global Education Monitoring Report VIEW database*. <https://education-estimates.org/out-of-school/data/>
4. Population Council (2025) *Evidence for Gender and Education Resource (EGER) website*. <https://popcouncil.org/evidence-for-gender-and-education-resource-eger>
5. Malala Fund (2021) *"Malala Fund makes commitments on girls' education at the Generation Equality Forum"*. <https://malala.org/newsroom/malala-fund-makes-commitments-on-girls-education-at-the-generation-equality-forum>
6. Malala Fund (2023) *Making the grade: Girls' education report cards*. <https://reportcards.malala.org/>
7. For activists, we understand quality funding to be multi-year, flexible and covers core costs. CHOICE (2023) *Written statement on youth-friendly funding*. <https://www.choiceforyouth.org/news/news-articles/press-releases/csw68-statement-on-youth-friendly-funding?acceptCookies=67a35d81607fa>
8. Adolescent Girls Investment Plan (2023) *Where is the Money? Funding adolescent girls and young feminist*. <https://adolescent-girls-plan.org/wp-content/uploads/2023/08/WD2023-Resourcing-Report.pdf>
9. Malala Fund (2023) *Making the grade: Girls' education report cards*. <https://reportcards.malala.org/>
10. Also see the Global Accountability Dashboard (<https://www.egeresource.org/global-accountability-dashboard/>) and the Global Platform for Gender Equality and Girls' and Women's Empowerment in and through Education (<http://www.unesco.org/sdg4education2030/en/knowledge-hub/global-initiatives/gender-equality-platform>)



